# MAMLUKI

Philipo Oyaro

©Philipo Oyaro, 2022

**ISBN 978-9987-9759-3-8**

Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kuchapisha, kunakili au kukifanyia maigizo kitabu hiki pasipo ruhusa ya mwandishi. Hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka agizo hili.

Riwaya hii ni ya kubuni, hivyo baadhi ya maeneo na majengo yaliyohusishwa hayana uhusiano na visa vilivyomo. Halikadhalika majina yaliyomo humu ni ya kubuni na huenda yakafanana na majina ya baadhi ya watu wanaoishi au waliofariki. Mwandishi anaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

**SHUKRANI**

Napenda niwashukuru waandishi Patrick J. Massawe na John Wisse, na rafiki yangu Jeremiah Machira kwa mchango wao mkubwa katika kuhariri mswada uliozaa riwaya hii. Na pia

Stanley Mwampulo, Lugendo Makumbati, Nicholaus Ntinika, na wakili msomi O.J. Kobas ambao kwa nyakati tofauti kompyuta zao zilitumika kuandaa kazi hii; bila kuisahau familia yangu kwa upendo wao katika kipindi chote nilipokuwa naandika kazi hii, na wengine wote walioniwezesha kwa hali na mali kutimiza ndoto hii—orodha ni ndefu. Mungu awabariki na awazidishie maradufu. Na kwa kipekee kabisa mwanangu Jason,

licha ya umri wake mdogo (miaka 10) alikuwa akinitia moyo nikae mbele ya kompyuta kuweza kukamilisha mswada wa kitabu hiki.

# 1

***Sud Kivu, DRC. Mei 7, 2015.***

Hukumu ilikuwa imesomwa. Pierre Businge na wenzake watatu walikutwa na hatia kwa mashitaka yote waliyotuhumiwa nayo: kupanga mauaji ya viongozi wakundi la *G23,* kutumiwa na serikali kusambaratisha kundi hilo.Na hukumu ilikuwa moja tu—kifo. Kifo cha risasi zisizo na idadi.

Wakati hukumu ikisomwa, Pierre Businge alikuwa ameuinamisha uso wake, akiyasimika macho ardhini. Lakini mara baada ya kusomwa hukumu hiyo aliuinua uso wake na kuyazungusha macho yake taratibu mithili ya kinyonga. Akawaona wapiganaji wenye silaha wakiwa wamelizingira eneo lote. Miongoni mwao walibeba makombora yenye uwezo wa kudungua ndege; wengine walikuwa na bunduki za kivita aina ya *AK 47.* Ukakamavu ulitawala japo kulikuwapo na wapiganaji ambao hawakuonesha kuzingatia vizuri itifaki za kijeshi.

Kisha macho yake yakamnasa mtu mmoja tu aliyekuwa amevaa kiraia. Hakuwa na bunduki wala

silaha yoyote kwa ajili ya kujilinda. Alielewa kwanini ilikuwa hivyo. Huyo alikuwa mwandishi wa habari aliyepenyezwa na makamanda ili aweze kuandika kwa kina juu ya tukio hilo; livifikie vyombo mbalimbali vya habari vya dunia, na kipekee kabisa, serikali jijini Kinshasa. Hiyo ilikuwa namna ya kuwatumia ujumbe kuwa wapo, kuwa hawaingiliki hata kama serikali ingepandikiza uasi miongoni mwao.

Macho yake yalihama na kuganda kwa Kanali Morison Ntaganda, kiongozi wa kundi hilo, na Luteni Kanali Bosco Nsangiyumba, naibu wake, waliokuwa wamesimama pamoja. Walikuwa ni walewale, sura zilezile lakini wakati huo sura zao zilikuwa zimevaa *ukauzu* uliopitiliza dhidi yake.

Shauku yake ya kuwa sehemu ya mchakato wa amani mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ikawa imetumbukia nyongo. Alikuwa akishangazwa na jinsi upepo ulivyobadilika ghafla. Watu walewale waliokuwa wakipambana pamoja naye, wakipanga mipango pamoja naye, wakila pamoja naye walikuwa wamemgeuka. Ilisadifu usemi kuwa rafiki wa leo adui wa kesho! Sasa walikuwa wamepata uhalali wa kumhukumu kifo, yeye na wapiganaji wengine.. Ilionekana kuwa azma yao hiyo imetimia.

Macho yake yakahama zaidi na kumnasa Jean Butembo, ambaye walikuwa rika moja. Kama wengine Jean alikuwa amevaa kombati na kofia iliyovutwa chini, akiwa mrefu kupita wote, na bunduki yake aina yaAK-47 ikiwa mkononi. Maumivu moyoni yalikuwa makali,

yakichochewa na kumwona Jean miongoni mwao. Huyu alikuwa miongoni mwa rafiki zake wa karibu. Naye alikuwa miongoni mwa waliomgeuka. Risasi kutoka kwenye bunduki ya Jean zingeutoboa mwili wake muda si muda kwa amri iliyokuwa imetolewa.

Historia ina kawaida ya kujirudia. Hii ilimkumbusha miaka mingi kabla. Ilimkumbusha mwaka 1994, kwao Rwanda katika kile kilichopewa jina, mauaji ya kimbari, wakati huo akiwa barobaro mwenye umri wa miaka isiyofikia hata kumi na mitano, ambako mambo yalikuwa hivyohivyo. Watu waliowafahamu kama majirani, watu walioishi nao, waliosali nao kanisani, wakiimba mapambio ya kumsifu na kumtukuza Mungu pamoja ndio walibeba mapanga, marungu na bunduki kuwashambulia, yeye akisalimika kimuujiza.

Akiwa mmoja wa makamanda wa kundi hilo, Pierre alikuwa na wazo la kuondokana na uasi, akaitikia wito wa Serikali jijini Kinshasa; wito wa kukomesha mapigano; wito wa kuketi kwenye meza ya mazungumzo. Wazo hilo likaonekana kuwa uhaini, usaliti, na hujuma dhidi ya kundi lake. Hoja dhidi yake ikaibuliwa. Alikumbuka jinsi mambo haya yalivyosukwa. Yeye na wenzake wanne walipoteuliwa kuongoza ujumbe wa G 23 kwenye kikao cha kutafuta kusitisha mapigano na maafisa wa jeshi la serikali ya Kongo,*Forces Armées de la République Démocratique du Congo (*FARDC). Kumbe alīkuwa akiundiwa zengwe. Majadiliano yakafanyika kwa dakika arobaini na tano tu ndani ya msitu mnene, ajenda ikiwa kusitisha mapigano

na kuangalia namna bora ya kulijumuisha kundi hili ndani ya FARDC. Ujumbe wa Pierre na wenzake hawakuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi isipokuwa kupeleka mapendekezo kwa makamanda wa G 23. Ujumbe wa FARDC ulioongozwa na Kanali Enock Mpiana, ambaye baada ya kikao aliomba kuteta na Pierre kwa dakika moja ulipata nafasi. Wakateta. Nongwa ikakolezwa hapo! Mmoja miongoni mwa wajumbe akaipenyeza hoja kwa makamanda huku akiwa ametia chumvi. Taarifa ikapokelewa kuwa kulikuwa na janjajanja ya kuwachuuza kinyume na matarajio yao.

Wenye kuitamani nafasi yake (wa tatu katika uongozi wa kundi) wakaishikia bango hoja hiyo, nyuma ya pazia ikiwa imetawaliwa na ubaguzi kutokana na asili yake ya kinyarwanda. Akajikuta amekuwa mhanga wa nia njema aliyoionesha. Hoja yake na wenzake wote waliokuwa wakimuunga mkono zikatajwa kuwa uhaini. Wakamvua cheo chake cha Meja na kumfungulia mashitaka.

Askari waliokuwa wamezingira eneo hilo walitoa nafasi upande mmoja. Pierre na wenzake, wakiwa wamefungwa mikono kwa kamba za katani, waliongozwa hadi kwenye miti, sehemu iliyokuwa maalumu kwa ajili ya kuwanyonga. Walifungwa mikono na miguu, mmoja baada ya mwingine. Kisha vichwa vyao, isipokuwa Pierre, vikafunikwa kwa mifuko myeusi. Hii ilikuwa katika kuhitimisha siku mbili za kuwa mahabusu, siku mbili zilizomzeesha, umbo zuri na umri wake wa miaka thelathini na mbili alionekana

kuzeeka kwa mwongo mmoja zaidi: uso umesinyaa, umepauka, macho yamezama ndani, mifupa ya shavu imechomoza; wakifungwa minyororo kwenye miti msituni, chini ya ulinzi mkali. Mikono ya Pierre iliuma, miguu iliwaka moto, kichwa kiligonga, njaa iliuma, kiu ndiyo usiseme! Hawakupewa chakula siku hizo mbili. Ilionekana kuwa hukumu yao ilikuwa ikitabirika hivyo ya nini kujihangaisha kuwalisha wakati wangenyongwa tu.

Askari kumi wenye bunduki, Jean Butembo miongoni mwao, walichukua nafasi zao yapata hatua thelathini kutoka walipofungwa Pierre na wenzake. Walilala kifudifudi ili waweze kulenga shabaha sawasawa. Zilitolewa amri kadha wa kadha za kijeshi. Yule mwandishi wa habari alikuwa makini sana kwa kila hatua. Alikuwa na kamera yake ndogo lakini yenye uwezo mkubwa wa kupiga picha, na alikuwa akipiga baadhi ya picha za matukio yaliyojiri hapo kwa umakini wa hali ya juu.

Kamanda wa zoezi hilo, mwenye cheo cha kapteni alisimama nyuma ya walenga shabaha na kupaza sauti, “Utaratibu wa ufyatuaji wa risasi ni kama ifuatavyo! Mnaanzia kushoto kwenu kwa kuwapiga risasi mfululizo na kuuchakaza mwili wake!Weka bunduki yako vizuri!”

Wapiganaji walielekeza bunduki mbele. Pierre aliyainua macho na kuyagandisha kwa Jean Butembo, akasonya taratibu.

“Lenga shabaha mbele… weka jicho lako kwenye dira ya shabaha!”

“Fyatua risasi!”

Mirindimo ya ushindani—*tyu!tyu!tyu!*kutoka katika bunduki hizo ilipasua anga kiasi cha kuyatatiza masikio ya wote. Risasi hizo ziliuchakaza mwili wa haini wa kwanza na kuacha harufu ya baruti ikielea hewani.

Kimya kifupi kilitawala. Pierre aligeuza shingo yake kutazama. Mwili ule ulikuwa umechakazwa kwa risasi, ilibaki kidogo tu ungekuwa kama chekecheo. Aliuinamamisha uso wake chini. Dakika chache zilizokuwa zinafuata naye zamu yake ingefika. Hakuwa na tumaini lolote la kuzuia hukumu hiyo kutekelezwa. Mwisho wake ulikuwa dakika chache mbele.

Mpiganaji mmoja kati ya wenye kutekeleza hukumu alienda kuhakiki hukumu ilivyotekelezwa na kuwaonesha wenzake ishara ya dole gumba; kuwa mambo poa.

“Haya, tuendelee na anayefuata…” alisema kamanda.

Hukumu kwa haini wa pili ilitekelezwa kama ya mwanzo. Hatimaye hukumu ikatekelezwa kwa haini wa tatu. Pierre aliwekwa wa mwisho kwa makusudi, yawezekana walipenda augulie machungu ya uhaini; machungu ya jinsi uhai ulivyowaondoka wenzake kwa namna ya kikatili. Mpiganaji aliyemkagua yule wa tatu na kuwapa wenzie ishara ya dole gumba, aliuchukua mfuko mweusi akamvisha Pierre kichwani.

“Haya, sasa tummalize huyu haini wa mwisho! Apigwe risasi za kutosha mpaka achakae kabisa, awe

kama chekecheo!" Kamanda huyo aliamuru kwa sauti iliyojaa dhihaka na majivuno.

Pierre alivuta pumzi na kuzishusha taratibu. Hakuwa na majuto tena ndani yake. Alikuwa amekubali yaishe, misuli yote ya mwili ikibana, tumbo likivuruga, mwili wote ukilowa jasho, akiihofia risasi ya kwanza na zingine ambazo zingeuchakaza mwili wake. Badala yake masikio yalinasa mirindimo zaidi. Hazikuwa zile bunduki. Ilikuwa mirindimo ya mabomu yaliyosikika kutokea pande zote za dunia. Alihisi maumivu makali shingoni, maumivu yaliyosambaa mwilini kote kama umeme. Kiza totoro kikatanda machoni mwake, akapoteza fahamu.

~~~

Taharuki ilitawala, kila mmoja akitenda kadiri akili yake ilivyomtuma.

Kundi hili lilikuwa limezingirwa na kushambuliwa na wanajeshi wasiowafahamu! Hawa walikimbilia huku, wale wakikimbilia kule. Mambo yalikuwa shaghalabaghala. Wapo waliokuwa wepesi wa kuziinua bunduki zao na kujibu mapigo, wapo ambao bunduki zilikuwa nzito wakashindwa kuzitumia, na njia rahisi kwao ilikuwa ni kuzibwaga na kutokomea msituni. Wapo pia ambao hawakuwa na bahati, wakioga risasi huku wakisakata rumba la kifo kabla ya kudondoka.

Dakika tano baadaye ukimya ulitawala eneo hilo, mapigano yakihamia sehemu nyingine. Milio ya hapa na pale ya bunduki bado ilisikika.
~~~

Yule mwandishi wa habari aliibuka kutoka alipokuwa amelala kifudifudi. Alikuwa amechakaa kwa kukanyagwa kanyagwa, damu katika nguo zake ikigandamana na vumbi, na kuwa kama kibaka *aliyegawanwa* na watu wenye hasira. Licha ya songombingo yote ile, alikuwa na kamera na kijidaftari chake kilichoandikwa matukio yote yaliyojiri. Akatokomea.

Jioni siku hiyo, katika vyombo vya habari vya ndani na vya kimataifa, habari kubwa ilikuwa kuuawa kwa Meja Pierre Businge, mmoja kati ya makamanda waandamizi wa kundi la *G23*. Picha kadha wa kadha na video fupifupi zilikuwepo mtandaoni kusindikiza habari hiyo.

Na katika vyombo vya habari nchini Kongo ilitangazwa taarifa ya kusambaratishwa kwa kundi la *G23* na *Forces Armées de la République Démocratique du Congo* (FARDC), Jeshi la Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

# 2

Akiwa ameketi kibarazani kwake, Changamwe, mjini Mombasa, nchini Kenya, Mohamed Mursal, almaarufu Mo, alikuwa akisikiliza Dira ya Dunia ya Idhaa ya Kiswahili ya BBC. Taarifa ya kuuawa kwa Pierre Businge ilimshitua, ikimtia simanzi huku machozi yakimlengalenga.

Mo alikuwa akimfahamu Pierre Businge, wakiwa wamefahamiana naye zaidi ya miaka saba. Pierre Businge alikuwa mmoja wa washirika *mahususi* mashariki mwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, katika biashara kubwa ya silaha na madini iliyokuwa imeshamiri eneo hilo. Bado Mo aliikumbuka siku ambayo Pierre aliokoa maisha yake miaka zaidi ya mitano nyuma. Siku hiyo alikuwa amelifikishamjini Uvira lori la mizigo kutoka Bandari ya Mombasa. Ndani ya lori hilo kulikuwa na shehena ya vipuri vya magari—ikiwa ndiyo bidhaa tajwa kwenye nyaraka za usafirishaji—pamoja na bunduki za kivita na risasi.

Alifanikiwa kushusha shehena ya vipuri vya magari. Shehena ya silaha ilikuwa ipokewe na watu wengine, chini ya usimamizi wa Pierre, umbali wa kilomita sitini toka Uvira. Shehena hiyo ilibadilishwa na kuwekwa katika gari jingine dogo.Muda mfupi baada ya kufika eneo la miadi, kuonana na watu wenye dili yao, alijikuta amezingirwa na kundi la wapiganaji.Akajua kwamba ameisha.

Wapiganaji wale hawakumsemesha. Walimshusha kutoka kwenye usukani, wakimsukasuka kwa kumsukuma na mara kadhaa kumpiga kwa vitako vya bunduki; wengine wakapita nyuma ya gari, wakikagua na kunong'ona, wakionekana kutikisa vichwa kuafiki, wakiongea haraka haraka kwa shauku. Kisha wakamtia pingu na kumpandisha garini upande wa abiria, usukani ukishikwa na mtu mwingine; gari likaondolewa. Baada ya mwendo wa dakika chache wakazama msituni; gari likafichwa. Wale wapiganaji wakaanza kuzishusha silaha na kuzificha msituni; jambo hili likifanyika kwa muda mfupi na wapiganaji waliojituma kama siafu. Kisha jambo la kuogofya zaidi likafuata. Alikabidhiwa mikononi mwa watu wawili ambao waliongea lugha asiyoifahamu lakini ujumbe uliokuwa umebebwa na lugha ile ulikuwa bayana. Watu wale waliamuriwa wamchukue na kwenda kummaliza. Gari dogo lililowabeba liliendeshwa taratibu na baada ya mwendo wa dakika kumi na tano hivi likasimama msituni. Akaamuriwa kuteremka. Alifunguliwa pingu na kuamuriwa kupiga magoti, mikono ikiwa kichwani.

Mmoja kati ya watu wale alikuwa na bastola mkononi. Yaonesha hawakutaka kutumia bunduki ambayo mlio wake ulikuwa mkubwa. Akaikoki!

Jasho lilimtoka Mo, kifo kilikuwa kimemkodolea macho; akafumba macho kusubiri. Mara ulisikika mlio wa bunduki. Risasi zikimiminika kama mvua. Mtu alidondoka nyuma yake, mwingine akikurupuka lakini hakufika mbali kwani alidondoka na kumfanya Mo kusikia kishindo na miguno ya maumivu. Mo aliganda kama gogo, amepigwa butwaa, macho yamemtoka.

"Una bahati sana!"

Sauti aliyoifahamu ilisikika nyuma yake.Uso ulibeba butwaa, akaganda, akili ikijaribu kufasiri kwa nguvu sauti hiyo.

"Pierre!"Mo alijawa na mshangao.

"Ni mimi ndugu,"Pierre alikuwa na bunduki, AK 47, mkononi,"tuondoke hapa upesi!"

"Wameuchukua mzigo wote!"

"Najua," alisema Pierrekwa utulivu akimrushia bunduki aliyoitwaa toka kwa watu wale. "Twende tukawatie adabu."

Walipanda gari lile lililomfikisha Mo mahali pale na kutelekezwa kilometa kadhaa toka mahali ziliposhushwa silaha. Kilichofuatia baada ya pale kiliripotiwa na vyombo vyote vikubwa vya habari vilivyofuatilia mzozo wa mashariki ya Kongo—mauaji ya wapiganaji thelathini katika mapigano ya makundi hasimu. Ambacho hawakufahamu ni kwamba hicho

hakikuwa kikosi cha wapiganaji bali washirika wawili waliojawa dhamira ya kuwatia adabu wanyang'anyi.

Tukio hilo liliimarisha ushirika wao na kufanya siku moja Mo ashushe ndege ya kijeshi iliyokuwa imesheheni silaha katika uwanja usiokuwa na usalama wa kutosha; uwanja uliokuwa chini ya Pierre na kundi lake.Akiwa rubani mzoefu, aliweza kurusha ndege hiyo kutoka jijini Mogadishu juu ya anga la nchi za Kenya, Tanzania na Burundi na kisha akatua salama na shehena hiyo ya silaha.

Taarifa aliyoisikia redioni ilimaanisha kuwa alipoteza mshirika muhimu katika biashara ya silaha na madini Mashariki mwa Kongo. Na taarifa kuwa jeshi la Serikali ya Kongo limesambaratisha kundi hilo la *G23* lilikuwa pigo kwa biashara hiyo.

Mo alikumbuka namna walivyokuwa wakiwasiliana ambapo mara nyingi waliwasiliana kwa baruapepe. Walikuwa wakiwasiliana kwa lugha ya mafumbo wakitumia majina bandia. Pierre alikuwa akijiita *Rita Twin,* huku Mo akijiita *Sabrina Sayeed.* Akiwa bado mwenye majonzi juu ya kifo hicho alifungua baruapepe ya mwisho kumwandikia Pierre kwa kutumia simujanja. Haikuwa na mambo mengi isipokuwa sentensi moja: *Heri ya mwaka mpya.* Hapa ilikuwa ni katika kutakiana heri ya mwaka mpya uliokuwa umeanza–ujumbe ambao ulijibiwa. Kabla ya kuifunga baruapepe hiyo alijikuta akiandika ujumbe mfupi: *Pumzika kwa amani, kifo chako ni pigo kwa harakati na ndoto tulizoota. Amin.*

# 3

Macho ya Pierre yalifunguka tena lakini ilikuwa kana kwamba mboni zilikuwa zikivutwa chini. Ubongo wake ulidurusu mifumo kadhaa ya fahamu—mwanga, ulaini wa godoro alilolalia, harufu ya dawa—lakini hakupata maana. Hakuwa akijua kilichokuwa kinaendelea.

Aliendelea kujilaza chali, mwili wake ukiwa dhaifu. Jitihada za kujongea zilimfanya ahisi maumivu mwili mzima.

“Pierre!” iliita sauti nzito, “Hatimaye umezinduka!”

Ilimchukua Pierre sekunde kadhaa kuichakata sauti ile iliyotoka jirani na kitanda. Wakati huu aliweza kuyafumbua macho yake na kuweza kumwona mwanaume aliyevaa fulana na jinzi.

“Pierre,” sauti nzito ya mwanaume huyu iliita kwa mara nyingine.

Wakati huu alimtambua, “Jean?” aliita, sauti ikigoma kutoka vizuri.

Tabasamu lilichanua usoni mwa Jean, “Una bahati sana.”

Pierre alijaribu kubashiri jambo gani lilitokea. Alikumbuka kuwa alikuwa amefungwa na kuvishwa tambara jeusi…kisha mirindimo ya risasi, maumivu, na kisha baada ya hapo kiza kinene kikitanda, akipoteza fahamu, pengine ndicho kifo chenyewe, na pengine hapo alipokuwa amelala kitandani alikuwa amefufuka. “Nipo wapi hapa?” aliinuka na kuketi kitandani. Maumivu hayakuwa makali ki-vile!

“Tulia, unahitaji kupumzika…”

Alikumbuka kuwa Jean alikuwapo miongoni mwa wale watimiza hukumu. “Jambo gani limetokea, nilipaswa kuwa nimekufa?”

“Lakini bado upo hai.Una bahati sana… siku yako ilikuwa haijafika. Niseme siku yetu wote, mimi na wewe.”

Pierre alimkazia macho. Kauli ile ilimchanganya.

Jean alionekana kumsoma vyema, “Kwanza nisamehe. Nilitakiwa kukupiga risasi. Sikuwa na namna isipokuwa kutii amri.”

“Najua, lakini imekuwaje nimeishia hapa?” alijitazama na ndipo akabaini kuwa alikuwa na bandeji mkononi, chini tu ya bega. Vidole vyake vilipapasa uso wake na kubaini uwepo wa bandeji. Uso wake ukatwaliwa na mshangao, *bandeji? Nini kilinijeruhi?* aliwaza.

“Kabla ya raundi ya mwisho, kabla ya kumimina risasi kulitokea uvamizi. FARDC walituvamia wakirusha mabomu na kusababisha mtafaruku, kila mtu alitawanyika kivyake. Ulijeruhiwa na mojawapo ya

mabomu yaliyorushwa, kipande kilichokupiga eneo la shingo.”

Mkono wa Pierre ulifika shingoni. Palikuwa na bandeji, na alipopaminya alihisi maumivu kwa mbali.

“Nilifanikiwa kutoroka,” alisema Jean, “na kisha kurudi eneo la tukio saa chache baadaye. Nilikuta maiti nyingi. Japo watu wetu wengi wameuawa nilikuwa na hisia kuwa ungeweza kuwa hai, kwani sikuwa nimefyatua risasi wala sikuwa nimesikia risasi toka miongoni mwa tuliokuwa tukilenga kutimiza hukumu.

“Nilipofika kweli nilikukuta bado ukiwa hai lakini ukiwa na majeraha na umepoteza fahamu. Nikakuchukua na kukuleta hapa.”

Pierre aliyazungusha macho yake tena kwenye chumba kile. Nyogeza iliyonasa macho yake ilikuwa ni bunduki—AK 47 iliyokuwa imeegeshwa ukutani. Aliweka umakini zaidi. Bunduki ile haikuwa tu AK 47, bali AK 47 aliyokuwa akiimiliki na kuitumia. Alimgeukia Jean, “Na hii ndiyo bunduki yangu ya siku zote?” mshangao uliuteka uso wake.

“Ndiyo yenyewe.”

“Imefikaje hapa? Maana nilinyang’anywa.” Hakuamini muujiza huu wa kuiona bunduki hiyo mahala hapo.

“Nilikuwa nayo mimi kabla ya shambulizi la FARDC kutokea.”

Pierre alitikisa kichwa katika hali ya kustaajabu. Miezi michache kabla, kwa ushawishi wa mmoja wa wapiganaji, walikwenda kwa mganga kwa ajili ya

zindiko. Bunduki yake pia ilifanyiwa zindiko huku mganga akimhakikishia hakuna atakayeweza kuiondoa bunduki hiyo mikononi mwake akaenda nayo. Na hata ikiondoka itarejea tu. Hapo alipo aliitazama. "Na hapa ni wapi? Je, Morrison na Bosco walisalimika?" Uchungu uliokuwa umeuteka moyo wake siku ile ya hukumu ulikuwa umeyeyuka.

"Tupo Bukavu… ni sehemu salama," Jean alimtoa hofu. "Bosco alisalimika lakini yeye na wapiganaji wengine walitiwa mbaroni na FARDC. Morrison habari zake sina, lakini huna haja ya kuwa na wasiwasi kwani baada ya mashambulizi yale inaaminika kuwa wewe ni miongoni mwa waliopoteza maisha. Vyombo vya habari vilitangaza habari hiyo. Serikali na Morrison, popote alipo, waliamini hivyo."

Pierre alivuta pumzi ndefu na kuzishusha taratibu, *kwa hiyo wanadhani kuwa nimekufa. Bosco yupo mikononi mwa dola na Morrison hajulikani alipo lakini yu hai.* Roho ya kisasi ilichomoza, *ngoja nipone.* Hakujua angelipizaje.

Miezi mitatu baadaye Pierre alikuwa amepona kabisa. Hakuwa na makovu, ngozi ilifunga vizuri na kurejea kuwa kama ya mtoto mchanga, isipokuwa makovu ya zamani pajani na ubavuni lakini alikuwa ameazimia kuondoka. Asubuhi moja alisafiri kwenda kusini hadi mji wa Uvira akiwa na begi dogo la mgongoni. Ndani ya begi hilo kulikuwa na AK47 na bastola.

Jioni moja akavushwa ki magendo kwa mtumbwi kuuvuka Mto Rucici unaotenganisha Jamhuri ya Kidemokarasia ya Kongo na Burundi. Burundi ilikuwa

ni njia tu ya kuelekea kule ambako moyowake ulipatamani—Tanzania.

Baada ya kusafiri kwa siku kadhaa, safari ya kuungaunga—mara kwa miguu, mara kwa bodaboda, mara kwa magari madogo ya abiria—akizikwepa mamlaka za ulinzi na usalama alifika mjini Muleba, mkoani Kagera. Alipumzika hapo kwa siku mbili. Akiwa hapo ndipo alijikuta akitamani kuingia kwenye mitandao. Alitafuta *internet café* na kufanikiwa kupata moja. Aliingia na kuperuzi mtandaoni, na alipofungua barua pepe yake akakutana na ujumbe ule uliotumwa na Mo, *Pumzika kwa amani, kifo chako ni pigo kwa harakati na ndoto zetu.* Naye akaijibu kwa ufupi sana, *Siku yangu haijafika.*

Siku ya tatu baadaye alipanda mashua kuelekea Gozba, mojawapo ya visiwa ndani ya ziwa Victoria, kuanza maisha mapya ya uchuuzi wa samaki. Miezi michache baadaye alijikuta anahamia kisiwani Kome, kunakopatika samaki wengi. Aliishi huko hadi serikali ilipoanzisha operesheni maalum ya kuwasaka wahamiaji haramu ndani ya visiwa vya Ziwa Victoria.

~~~

Mawimbi yalisikika yakigota ufukweni. Hali ya hewa ilikuwa ya baridindani ya kibanda kidogo cha wavuvi kilichojengwa kwa vipande vya maturubai. Pierre Businge alijikunyata juu ya mkeka, akijifunikagubigubi kwa shuka la kimasai kujisitiri dhidi ya baridina mbu wengi waliokuwa wakimzengea ili waifaidi damu yake.
~~~

Kando yake walikuwapo wachuuzi wengine kama yeye, pia wakiwa wamejifunika gubigubi, wakikoroma kwa kupokezana kama vyura wa majarubani. Haya ndiyo yalikuwa maisha yake ya uchuuzi wa samaki. Alikuwa akisubiri kuwasili kwa wavuvi, alangue samaki kisha awauzie wachuuzi wengine. Alikuwa amefanya hivyo zaidi ya miezi sita tangu ahamie kisiwanihumo.

Usiku uliotangulia alikuwa amechelewa kulala sababu ya muziki wa dogoli. Aliupenda muziki huo ambao haukufanana na muziki wa rumba aliouzoea, muziki aliouimba. Muziki huu wa dogoli ulikuwa wa kasi, wanawake kwa wanaume, wasichana kwa wavulana wakinengua kwa kasi, wakipandisha hanjamu. Muziki uliomfanya achelewe kulala na kujikuta asubuhi akiwa ndani ya shuka.

Pierre alikurupuka kutoka usingizini kufuatia zogo lililokuwa likiendelea. Wavuvi walikuwa wamewasili. Alilikunja shukalake na kulitelekeza juu ya mkeka na kuharakisha ilikotia nanga mitumbwi ya wavuvi huku akichomoa burungutu la notitoka mfuko wa suruali. Kabla hajaifikia ile mitumbwi alitokea mfanyabiashara mwenzake aliyemvuta kando kumnong'oneza jambo.

Pierre hakuweza kuuona uso wake sababu ya mwangaza hafifu wa alifajiri lakini sauti yake ilionesha kuwa na hofu. "Vipi mbona kama una wasiwasi?"

"Naondoka."

"Unaondoka?" Pierre alihoji,"Unaondoka kwenda wapi wakati sasa ndiyo biashara imechanganya?"

"Kwani hujasikia?"

“Kusikia? Kusikia nini?”

“Wanasaka wahamiaji. Sina kibali.” Huyu lafudhi yake ilimshitaki bila chenga kwamba ni mrundi. “Na wewe huondoki?”

Swali hili lilimgutusha Pierre akakunja uso. “Kwenda wapi?”

Akishusha sauti na kusema, “Kila mtu hapa anajua wewe ni mnyamulenge.”

Kauli hii ilimkata maini, ikaunda mwangwi mkubwa ndani ya ubongo wake. *Kila mtu anajua wewe ni mnyamulenge. Kila mtu anajua…Hapa kisiwani si salama tena,* aliwaza. Siku zote alikuwa anadhani kuwa hafahamiki kumbe alikuwa anajidanganya tu; watu walikuwa wanamchora tu. Taharuki ikauteka ubongo wake. Kasi ya mapigo ya moyo ikaongezeka, vitone vidogo vya jasho vikijiunda usoni licha ya ubaridi uliokuwapo. “Kwa hiyo unaondokaje?” aliinua macho kumtazama mtu yule mwenye lafudhi ya kirundi.

“Naondoka kwa boti inayopakia samaki pale.” Alielekeza kidole ziwani kulikokuwa na mashua kadhaa.

“Unakwenda wapi sasa?” Pierre alisahau kuwa alikuwa pale kwa ajili ya uchuuzi wa samaki.

“Mwanza?”

“Mwanza?” Pierre alichanganywa na jibu lile.“Kwani huko msako haufiki?”

“Ule mji mkubwa, nikifika huko nitajua cha kufanya.”

Alipoagana na mtu yule alikutana na mwingine; na mwingine. Simulizi ilikuwa ni ile ile—serikali inafanya

msako wa wahamiaji haramu, muda wowote wangetua kisiwani pale.

Simulizi mbili-tatu zilionesha kuwa misako hii huwa noma; huwa sagurasagura na fagiafagia, ikikumba waliomo na wasiokuwamo. Simulizi hizi ziliotesha mbawa shughuli yote ya uchuuzi wa samaki na kuamua kuchukua bodaboda kumpeleka kwake.

Aliteremshwa yapata mita ishirini toka nyumba aliyokuwa akiishi. Haikuwa nyumba ya maana sana; ikijengwa kwa tofali za saruji bila ya kupigwa ripu, na ilikuwa imezungushiwa ua wa matete. Ilikuwa ni ya chumba na sebule. Hapa aliishi peke yake.

Alipoingia ndani wenge lilikuwa maradufu hasa alipozikumbuka silaha alizovuka nazo mpaka—bastola na bunduki, AK 47, alizokuwa amezificha ndani ya nyumba hiyo. Hakuwahi kuzikagua wala kuzigusa. Sasa wenge lilikuwa wapi pa kuzihifadhi, hasa ile AK 47. Kwa bastola isingekuwa shida. Wakati akibangua bongo aliingia chumbani na kuzama mafichoni, kwenye kishimo sakafuni kilichofunikwa kwa zulia na kuwekwa kabati la nguo juu yake. Aliondoa kifuniko na baada ya jitihada za sekunde chache aliibuka na mfuko wa sandarusi.

Alitoa bunduki ya kivita, *AK 47,*na bastola ya kijeshi aina ya *Mugnum 66mm.* Aliziweka mezani silaha hizo. Hakuna aliyewahi kuziona silaha hizo ambazo hakuwa na nia ya kuzitumia katika ujambazi.Alikuwa mpiganaji na siyo jambazi, na habari ya kufanya ujambazi haikuwahi kuingia akilini mwake. Kuja kwake kisiwani

hapo ilikuwa kutafuta utulivu na amani ya moyo. Hakuwa na mali nyingine aliyomiliki tofauti na fedha aliyokuwa akizungusha katika biashara na akaunti ya benki, iliyonona katika Benki ya Federal. Fedha zilizotokana na dili zake za awali alipokuwa Kongo.

Aliifungua bastola na kuitawanya mezani kisha akaanza kuisafisha kipande kimoja baada ya kingine kwa uangalifu mkubwa kama aliyekuwa akisafisha mboni ya jicho. Alipokuwa ameridhika alipanga tena. Akaijaza risasi akaijaribu mkononi."Hapa sawa," alinog'ona. Alizirejesha silaha zote ndani ya sandarusi na kisha mafichoni.

Siku hiyo nzima alijilaza, akitoka tu wakati wa chakula cha mchana, na kisha kurejea. Aliwasiliana na mmoja wa marafiki waliokuwa wamefahamiana kwa kipindi kifupi kisiwani hapo, amsaidie kupata mashua ndogo ya kukodi kumpeleka jiji Mwanza.Kiza kilipoingia alitoka na jembe, akachimba shimo upenuni mwa nyumba, kiasi cha mita moja, akitweta, kijasho kikimtoka. Alirejea ndani na kutoka na kisandarusi kilichokuwa tu na bunduki huku akiwa amekata shauri ya kubaki na bastola.

Ilikuwa ni wiki mbili tu tangu alipe kodi ya miezi mingine mitatu; hivyo kutokuwepo kwake kungekuwa hadi upepo huo mbaya utakapotulia. Alipanga kumjulisha mwenye nyumba kutokuwepo kwake ili amtunzie nyumba pale atakapokuwa ameondoka kisiwani hapo.

Safari ilianza saa mbili usiku. Wenye mashua, walishachukua chao, hawakujua kwanini Pierre alikuwa ameamua kukodi mashua kumpeleka Mwanza usiku huo. Ilikuwa ikitokea mara chache lakini halikuwa jambo la kushangaza.

# 4

*MWANZA, Desemba 10, 2015.*

Wingu zito lilikuwa limetanda angani mithili ya blanketi zito jeusina kusababisha kiza totoro japo taa za umeme toka majengo mbalimbali zilijaribu kupambana na kiza kile. Bila hata ya kuambiwa, Pierre alibaini kuwa wanakaribia kufika kwani kwa mbali ziwani walilakiwa na taa za umeme zilizotapakaa mbele yao; taa zilizosadifu sura ya nchi, sura ya Jiji la Mwanza na viunga vyake iliyotawaliwa na milima na maghorofa.

Nahodha alizima injini, mashua ikapunguza mwendo. Walikuwa wanahitimisha safari ya saa nne majini, safari iliyotawaliwa na ki ubaridi cha ziwani. Ilikuwa ni bahati njema kwa Pierre kwamba alikuwa amekumbuka kuvaa jaketi lililomkinga na ki ubaridi hicho.

Saa sita juu ya alama usiku, mashua hiyo ilitia nanga Kirumba Mwaloni Jijini Mwanza. Kushoto mbele yao kulikuwapo jengo kubwa la soko. Usiku huo hakukuwa na shughuli zozote zilizokuwa zikiendelea. Palikuwa

tulivu. Mijongeo iliyokuwapo ilikuwa ni ile ya walinzi, baadhi wakiwa na sigara mdomoni.

Mashua hiyo ilitia nanga takribani mita tano kutoka nchi kavu. Nahodha alijaribu kina cha maji kwa kasia, kisha alimgeukia Pierre, “Kina cha hapa kifupi, unaweza kushuka.”

Pierre alilazimika kukunja suruali hadi magotini huku akivibeba viatu vyake kwa mkono wake wa kushoto. Mkono wake wa kulia ulikuwa umeshika mkanda wa begi dogo la mgongoni, akashusha miguu. Maji yalimfikia magotini. Yalikuwa na joto tofauti na kiubaridi kilichokuwa kikipuliza. Alipofika nchi kavu, aliikung’uta miguu yake kuondoa mchanga; akakunjua suruali, kisha akavaa viatu. Alibaini uwepo wa mitumbwi mingine iliyokuwa imetawanyika pale ufukweni, ambapo watu wawili-watatu walikuwemo ndani ya mitumbwi hiyo.

*Sasa nitafute sehemu ya kulala,* aliwaza. Ulitanda ukimya isipokuwa sauti ya mawimbi madogo yaliyokuwa yakigonga ufukwe huo wa Ziwa Victoria. Kwa mbali sauti za muziki wa *dogoli* ulipasua anga, ukamkumbusha usiku uliotangulia alivyochelewa kulala akinengua lakini huo haukuwa wakati wa kunengua.

Alipepesa macho yake kushoto na kulia, nyuma na mbele; taa za majengo ya jirani zilimulika njia na kubainisha kuwa alikuwa mwenda kwa miguu pekee barabarani usiku huo. Ukimya ulitawala, akizisikia

nyayo zake mwenyewe. Alitamani asizisikie kabisa nyayo zake, pawe kimya kabisa, mithili ya kivuli kinachojongea sababu hakutaka kumgutusha mtu yeyote. Hapa na pale alipishana na magari machache yalimpita na kumulika barabara hiyo. Baadhi yalikuwa na mwanga mkali uliomchoma machoni, na mara kadhaa alilazimika kutumia mikono yake kuyakinga macho yake.

Hii ilikuwa mara yake ya pili kuwa jijini Mwanza. Mara ya kwanza ilikuwa yapata miezi mitano nyuma, alipokuwa amefika mjini kusuuza macho. Simulizi za wachuuzi wenzake kisiwani zilikuwa zimemjengea shauku ya kuyaonja hayo maraha ya mjini  na kujikuta amefikia Lake Hotel, iliyopo Barabara ya Stesheni, katikati ya jiji.Mara hii nafsi ilimtuma kwenda kulala hukohuko. Tofauti na usiku huu, siku ya kwanza alifika mchana na alikuwa na mwenyeji. Alitaraji kupata teksi au bodaboda ya kumpeleka huko, lakini hakukuwa na teksi iliyopita kwa wakati huo. Na hata bodaboda mbili-tatu zilizopita zilikuwa na abiria.

Dakika sita zilikuwa zimepita tangu ateremke kwenye mashua. Akaongeza mwendo hasa pale alipokutana na kibao kilichosomeka *Barabara ya Makongoro*. Hisia zilimtuma kuwa hiyo huenda ikawa ni moja ya barabara kubwa. Idadi ya magari, japo kwa mbali, ilikuwa kubwa kulinganisha na ile ya barabara aliyokuwapo, na huenda ingekuwa rahisi kupata teksi au bodaboda ya kumsogeza aendako.

Akiwa amebakiza mita chache kuifikia barabara ile, ghafla kutoka kizani, aliibuka mtu kushoto kwake. Nywele zikamsimama, mapigo ya moyo yakiongezeka maradufu yakisindikizwa na kijasho chembamba. Aliganda misuli imekaza, tayari kutoka nduki. Kabla hajajua nini kinaendelea, kabla hata ubongo wake haujalipokea hilo, aliibuka mtu mwingine kulia. Wakamzibia njia!

King'ora cha hatari kilipaza sauti kichwani mwake. Hakuhitaji kuambiwa kuwa hao walikuwa vibaka waliokuwa wamemweka kati ili kumpora. Kwa hadhari kubwa aliigeuza shingo yake kule alikotoka, kutafuta namna ya kujinasua lakini kwa mshangao huko nako kulikuwa na watu wengine wawili na kuifanya jumla yao kuwa wanne, wakiwa na jambo lao. Alivuta pumzi na kuzishusha taratibu, *hapa ama zangu ama zao,* akapiga moyo konde.

Japokuwa kiza kilikuwa kimetanda na kutoweza kuwaona vizuri, aliweza kuhisi kuwa watu hao, ambao kwa vyovyote vile hawakuwa wema, walikuwa wamebeba silaha. Kama siyo mapanga au visu, basi ni marungu au vipande vya nondo. Alibaki amesimama kama sanamu lililosimikwa katikati ya barabara, moyo ukidundia masikioni. Watu wale walikuwa kama vile wanategeana, kuona nani atalianzisha. Nukta kadhaa zikakatika—kimya!

Kisha upesi, bila ya kuwagutusha vibaka hao, alijipapasa kibindoni kuchomoa bastola. Akaikoki huku ikitoa mlio—*kliki*; mlio uliosababisha mmoja wa vibaka

hao kuwasha kurunzi yenye mwanga mkali na kummulika.Kibaka mwingine aliyekuwa upande mwingine aliliinua panga lake ilikumshambulia.Pierre aliliona shambulizi hilo na kwa silika ya mnyama akakwepa. Hii ilikuwa vita. Ilionesha dhahiri kuwa watu hao hawakuwa na nia tu ya kumpora mali isipokuwa kumpora vyote—mali na roho.

Kufumba na kufumbua, Pierre aliachia risasi moja iliyompata kifuani yule aliyemshambulia. Mvumo wa bastola hiyo ulivunja ukimya uliokuwa umetawala eneo hilo ukifuatiwa na yowe kali la maumivu naukelele wa kudondoka kwa panga kwenye lami. Nukta hiyohiyo mwanga mkali wa taa za gari lililokuwa limepinda barabara hiyo ya Mwaloni kutokea Barabara ya Makongoro uliwamulika.

Vibaka hao walitimua mbio na kutokomea gizani,kila mmoja kwa njia yake kama panya waliokurupushwa na paka wakiwahi shimo lililokaribu. Wakimuacha mwenzao amedondoka, akiipigania roho yake.

Pierre alipigwa butwaa kwa sekunde chache, bastola mkononi. Gari lile likimsogeleakwa kasi bila ya kufanya jitihada za kumkwepa. Alililikwepa na kujaribu kutokomea gizani lakini alikuwa amechelewa. Gari hilo, Toyota Land Cruiser, lilifunga breki karibu yake, askari wa jeshi la polisi, wenye silaha wakichupa kutoka garini. Mambo mawili yangeweza kutokea—kupigwa risasi au kukamatwa. Hilo la kwanza lilimwogofya.

Alitambua kwamba yupo hatarini kutiwa mbaroni kuliko wakati mwingine wowote tangu aingie katika

nchi hii. Kuwaruhusu askari hao wamtie mbaroni ilikuwa kuzima ndoto zake zote, kwani ambacho kingefuata ni kifungo jela. Idadi ya makosa ambayo yangemtia hatia ilikuwa imeongezeka kutoka kuishi nchini kinyume cha sheria, kupatikana na silaha ya moto, hadi mauaji yalitokea kitambo. Kwa uzoefu wake risasi iliyolenga sawasawa aliifahamu. Ile aliyoifyatua ilikuwa imemlenga sawasawa kibaka. *Sitawaruhusu wanikamate,* aliiambia nafsi yake. Alitimua mbio akiandamwa kwa kasi na askari.

Ilikuwa dhahiri kuwa asingeweza kumzidi mbio askari huyo. Kifua kilichemka, pumzi zikamwenda mbio. Vishindo vya miguu vilimkaribia. Ghafla aligeuka na kumfyatulia risasi mbili askari aliyekuwa akimfukuza. Risasi iliyolenga aliifahamu. Moja kati ya risasi hizo ilimpata askari huyo akapiga yowe la maumivu.

Pierre akatokomea gizani. Hakukuwa na vishindo nyuma yake. Majanga yaliyokuwa yakimwandama hayakuwa na kikomo. Zile fikra kuwa sasa angeweza kuwa salama zilizima ghafla kama mshumaa kwenye tufani. Jiji la Mwanza lililokuwa limetoa matumaini kuwa sehemu salama, sehemu ya kujificha, sehemu ambayo angeendelea na maisha yake bila kuhisiwa kirahisi kuwa mhamaji haramu lilikuwa limemsaliti. Mwanza haikuwa sehemu salama tena kwake. Alipaswa kuondoka kabla ya polisi hawajaanzisha msako mkali ambao ungemtia mbaroni. Jibu la muda mrefu halikuwapo, lakini jibu la muda mfupi lilikuwa miguu

yake—kukimbia kwa kadiri miguu hiyo ingeweza kumbeba.

~~~

Alikimbia kadiri miguu yake ilivyomruhusu, akiifuata barabara nyembamba iliyokuwa na madimbwi ya maji. Mara kadhaa alijikuta akiyapamia madimbwi hayo na maji kumrukia hadi usoni lakini hakumpunguza mwendo. Dakika chache baadaye alitokeza kwenye barabara ya lami. Mwangaza wa taa za barabarani uliangazia eneo hili. Tofauti na kwingineko alikopita, mtaa huo ulikuwa umechangamka, watu kadhaa wakiwepo barabarani huku teksi na bodaboda zikiwa zimeegesha kusubiri wateja.

Pierre alisitisha mbio, akaiswinda bastola yake kibindoni akiifunika vizuri kwa shati na jaketi. Alitembea kwa hadhari jasho likimtoka, koo limemkauka, akikatiza kulipokuwa na mwanga mkali. Madereva teksi na bodaboda walimtamani, wakajaribu kumshawishi kuchukua usafiri. Mithili ya mtu aliyetia pamba masikioni, hakugeuka wala kupunguza mwendo.

Pande mbili zilizopakana na barabara hiyo, kulikuwa na kumbi mbili za starehe. Kushoto kwake juu, toka kwenye bango liwakalo taa, maandishi—Villa Park Resort—yaliyosomeka, huku masikio yake yakinasa mdundo mzito wa muziki wa rumba toka humo.

Hapo palikuwa na magari mengi yameegeshwa. Upande wa nje kulikuwa na dadapoakadhaana makuadi wao waliokuwa wakijipitisha hapa na pale wakiwa
~~~

mawindoni. Pierre akavuka eneo hilo, na kushoto kwake palikuwa na ukuta mrefu wenye milango mingi, taa za umeme zikiwaka juu ya kila mlango, na alipatafakari akahitimisha kuwa ulikuwa uwanja wa mpira.

Taa zile ziliangazia barabara, na kisha kwa mbele giza likitawala. Pierre aliongeza mwendo kulifuata giza lile kwani alihitaji giza kuliko mwanga. Kwa mbali nyuma yake mwanga mkali wa taa za gari lililokuwa likija ulimgutusha, akaanza kutimua mbio tena na kutokomea kizani zaidi hadi alipokutana na mwinuko. Taa ziliashiria kuwa nyumba za eneo hilo zilikuwa zimejengwa mlimani. Haikumchukua muda mrefu kubaini kutokuwepo njia iliyonyooka.

Alijikwaa kwenye jabalina kula mweleka lakini alijizoa, macho yake yakilizoea giza na kubaini uwepo wa majabali, na kuendelea kuparamia majabali. Baada ya dakika kumi, akiwa anatweta alijikuta amekwea hadi juu. Alipogeuka kutazama alikotoka. Aliona taa za baadhi ya maeneo ya katikati ya jiji kwa mbali. Aliendelea kuifuata njia ndogo iliyokuwa na majabali pande zote. Aliibukia kwenye kijumba cha slopu.Taa katika mojawapo ya chumba ilikuwa ikiwaka, ikipenyeza mwanga kupitia nyufa mlangoni. Alisita pale harufu kali ya bangi ilipozigonga pua zake. Harufu ile ilimtahadharisha kuwa ameingia himaya nyingine; himaya ambayo wenyewe walifanya watakavyo ikiwa ni pamoja na kuvuta bangi bila hofu ya mamlaka za dola. Macho yake yalipozoea mwangaza hafifu wa eneo hilo yalimnasa mtu aliyekuwa ameketi juu ya jabali. Mtu yule alivuta

pafu jingine, mwangaza mwekundu wa msokoto ukauangazia uso wake, kisha akaachia moshi mzito uliokoleza kiza.

Alimsogelea mtu yule.“Habari za usiku ndugu…”

Zilikatika nukta kadhaa ndipo akajibu, “Nzuri.” Sauti yake ilikoroma kama spika mbovu yenye kufuga mende.

“Samahani ndugu, mimi ni mgeni hapa, naomba kuuliza.”

“Mgeni?”Alipiga pafu na kuuachia moshi kumwelekea Pierre.

“Ndiyo.” Harufu ili ilimtatiza lakini akajikaza kisabuni. Maishani mwake aliwahi kujaribu *hiyo kitu*lakini akaachana nayo.

Mtu yule alivuta pafu jingine. “Umetokea wapi?” aliubana moshi na kuuachia taratibu, akikung’uta jivu toka msokoto wake.

Pierre alisita kidogo, akiwa njiapanda, hajui aeleze ukweli au la. Mwishowe akafunguka “Nimetokea Kome…”

“Kome… Kome… aa! Kule kisiwani!”

“Ndiyo.” Pierre alinong’ona.

“Wewe ni mvuvi?”

“Hapana, ni mchuuzi wa samaki…”

“Ehee, sema shida yako.” Alivuta pafu jingine na kumpulizia moshi.

Kitendo hicho kiliashiria dharau, jeuri na kiburi lakini alikitafsiri kwa mtazamo chanya; tafsiri kwamba mtu huyo ni alwatani eneo hili, kwamba anaweza kumpa hifadhi, kwamba ni mhalifu kama wahalifu wengine na

anazijua chocho. “Ninaweza kupata sehemu ya kulala kwa usiku huu?”

“Ahaa! Huku milimani huwezi kupata vyumba.” Mtu huyo alichekea tumboni.“Wewe si umetokea huko chini?”

“Ndiyo, nimetoka huko…”

“Basi, rudi hukohuko ndiko utapata nyumba ya wageni,” alivuta pafu jingine, akaubana moshi na kisha kuuachia taratibu. “Zipo gesti nyingi tu na huduma hadi saa hizi zinapatikana.”

“Ah! Nimechoka kweli. Mpaka nirudi huko?” Kurudi kungemaanisha uwezekano wa *wajuba* aliowatoroka kumtia mbaroni. Na kwenda nyumba ya wageni ilikuwa sawa na kujikabidhi mwenyewe kwani kwa vyovyote vile msako ungefanyika kubaini wageni.

“Alaa! Sasa nikusaidiaje?”

Ukimya mfupi ulitawala Pierre akaamua kujivua unyonge, “Nahitaji pa kulala. Nitakulipa…”

Ilikuwa zamu ya mtu yule kuwa kimya. Uso wake ulitiwa wekundu wa pafu moja la nguvu na kuachia moshi mzito.

“Poa, sehemu ya kulala itapatikana. Unategemea kulala siku ngapi?”

Swali hili lilimtatanisha. Kujikuta kwake hapa ilikuwa dharura. “Nitalala kwa siku mbili…yaani usiku wa leo na kesho.”

“Poa, utanipa shilingi elfu ishirini.”

“Hakuna shaka.”

Mtu huyo alinyanyuka toka kwenye jabali na kimo chake halisi kuonekana. Alikuwa wa kimo cha wastani.

Kwa mbali angetajwa kuwa mfupi, lakini ameshibashiba. “Njoo ukiangalie, kuna kitanda na godoro...”

Pierre alimfuata.

Mtu yule alifungua mmojawapo ya milango na kuwasha taa.Palikuwa na kitandani cha mbao, futi nne kwa sita, kilichokuwa na godoro kuukuu, chandarua chenye matobo kikining’inia. Pierre aliridhika na kwa kiasi fulani alifarijika kuwa hapo.

“Vipi, kiko poa?”

Macho yake yalikitathmini chumba kile. “Kiko poa.” Kisha akayarejesha macho kwa mtu huyo. Macho yake yalikuwa mekundu, meno yameungua, pua bapa kama vile iliwahi kubamizwa na kushindwa kurudi. Kichwani alinyoa nywele zote na kubakia upara, akiwa na kovu juu ya sikio la kulia akionesha kuwa alishawahi kushonwa nyuzi kadhaa.

“Mimi naitwa Makubi.” Alijitambulisha “Sijui wewe unaitwa nani?”

“Rish Kabasele.”

Pierre alilipa kiasi walichokubaliana. Makubi alikipokea na kukisunda mfukoni.

“Ngoja nikuangalizie shuka.” Makubi alitoka chumbani mle na kurejea na shuka mbili za rangi ya pinki.

Makubi alipoondoka Pierre alitandika kitanda chapu. Hakuvua nguo zote isipokuwa jaketi. Kuvua nguo kungemtenganisha na shilingi milioni tatu alizokuwa amehifadhi maeneo mbalimbali katika nguo hizo. Alivua

viatuhuku akiiweka bastola chini ya mto, akazima taa na kujitupa kitandani.

Haikuwa rahisi kupata usingizi, hasa baada ya matukio ya usiku huo. Alijigeuzageuza kitandani huku matukio yote ya siku ile yakijirudia kama filamu kichwani mwake: asubuhi taarifa ya msako wa wahamiaji haramu, safari ya saa nne ziwani, na kubwa zaidi matukio ya usiku huo. Mara ya mwisho kurusha risasi na kuutoa uhai wa mtu ilikuwa ni zaidi ya miezi saba katika harakati  mashariki ya Kongo. Kisha akajilaumu kwa maamuzi yake ya kusafiri usiku. Pengine ingekuwa mchana haya yote yasingetokea, pengine angekuwa sehemu tulivu amelala fofofo. Lakini usiku huu alikuwa kwenye chumba hiki chenye godoro lenye kunuka uvundo, akijutia maamuzi yote aliyoyafanya kabla.

Baada ya kujigeuzageuza kwa zaidi ya saa mbili, akihesabu bati na mbao darini, usingizi ukampitia.

Pierre alishituliwa na jogoo aliyewika kuashiria mawio. Aliamka na kuyazungusha macho yake akivuta kumbukumbu, ndipo alipokumbuka kuwayupo ndani ya nyumba aliyopewa hifadhi. Saa yake ilimwonesha ilikuwa imetimu saa kumi na mbili za asubuhi. Usingizi ulikuwa bado umembana kutokana na uchovu mwingi, akajirudisha tena kitandani. Matukio yote yaliyotokea usiku yalikuwa bado mabichi ndani ya ubongo wake. Aliendelea kujilaza huku akipanga na kupangua kichwani mwake. Alipojitazama nguo zake zilikuwa

zimechafuka na zimekunjamana kama zimetafunwa na ng'ombe.

Alipoamka alizitwaa buti zake kutoka uvunguni mwa kitanda huku macho yake yakiganda lilipo begi lake la mgongoni. Aliitwaa bastola toka chini ya mto na kuitia ndani ya begi akabaki akishindana na nafsi yake, aondoke na begi lake au aliache humo chumbani hadi jioni atakaporudi? Alichagua kuliacha humo chumbani. Alibadili nguo na kuvaa zingine—fulana na jinzi—bila hata ya kwenda kuoga kwani kwenda kuoga katika bafu la nje na kisha kurudi ndani haikuwa salama kwake. Alitamani akichomoka hapo iwe ni kama mshale, majirani wasije kumwona na kujiuliza maswali ambayo yangemtia matatani. Alihamishia fedha zake kwenye mifuko ya jinzi.

Alipotoka njehakumkuta mwenyeji wake, Makubi, pengine alikuwa ameshaondoka muda mrefu kwenda kwenye shughuli zake.Alipata fursa ya kuitazama nyumba hiyo kwa nje. Ilikuwa ni nyumba ya vyumba vinne, kimoja alicholala yeye na vingine vitatu ambavyo kila kimoja kilikuwa kimetiwa kufuli. Aliufunga mlango kwa kufuli alilolikuta chumbani mle akautia ufunguo mfukoni. Akashuka akikifuata kinjia alichopanda nacho usiku wa manane, ki njia chenye majabali pande zote.

Alipoyaacha majabali yale aliuendea uelekeo wa kushoto. Alitembea hadi alipoifikia barabara ya lami. Huko alikutana na daladala zilizokuwa zikifanya safari kati ya Ilemela na Kisesa. Hakujua chochote kuhusiana na maeneo hayo zaidi ya kusoma maandishi kwenye

magari hayo ya abiria. Hakutaka kuuliza, isipokuwa kupanda moja ya magari hayo akiwaza kuwa kama mwelekeo utakuwa sio ule anaoutaka basi angeteremka na kuelekea kwingine. Daladala ilipofika kituo cha daladala, Pasiansi, abiria kadhaa walipoteremka, naye akateremka.

Upande wa pili wa barabara kulikuwa na hoteli moja iliyomvutia, iliyokuwa katika jengo la ghorofa nne. Alisubiri magari yalipokuwa yamekata, akavuka kuifuata.

Alifikia kwenye ukumbi wa baa uliokuwa na kaunta ya vinywaji huku meza kadhaa ndani ya ukumbi huo zikiwa zimejazwa na wateja waliokuwa wanapata kifungua kinywa, bakuli za supu na chapati zikiwa mbele yao, wengine mayai, kahawa, chai. Harufu ya mahanjumati ilitawala. Pierre aliagiza supu ya kuku, chapati na kahawa. Huu ulikuwa mchangayiko ambao hakuwahi kuufanya—kunywa kahawa na supu kwa wakati mmoja lakini alishawishika baada ya harufu nzuri ya kahawa iliyokuwa kati ya harufu nzuri iliyojaza eneo hilo. Alipokuwa ameshiba alimwita mhudumu na kumwagiza bia aina ya Balimi.

Aliinywa bia ile huku tukio la usiku likirejea kichwani, akitafakari juu ya usalama wake, akitafakari hatua nyingine ya kuchukua. Kubwa lililokuwa likizunguka kichwani mwake ni kuondoka na kwenda kwingineko ambako kungekuwa salama kwake.Swali likabaki ni wapi pa kwenda? Hakufahamu! Aliinywa bia ile taratibu. Taratibu kanakwamba alikuwa akiidai majibu.

Alipokosa jibu kwenye chupa ya kwanza aliagiza ya pili na ya tatu. Zote zilikuwa kimya. Hazikumpatia majibu.

Wakati hayo yakiendelea kichwani mwake, aliwachokoza kwa ofa ya vinywaji, wanawake wawili waliokuwa wakipata supu. Haikupita muda wakajikuta wapo meza moja iliyosheheni vinywaji. Wanawake hao wenye umri wa miaka thelathini na ushei. Muda mrefu ulikuwa umepita tangu mara ya mwisho kujikuta katika mjumuiko na wanawake warembo.

Mmoja alikuwa mwembamba, amevaa blauzi iliyoyaacha mabega yake wazi. Shingoni alivalia mkufu wa dhahabu na hereni za dhahabu masikioni, nywele zikitiwa rangi ya dhahabu. Japo ilikuwa asubuhi, alionesha hali ya kukolea kilevi, ishara kuwa hakuwa ameaanza asubuhi hiyo bali kukesha akigida vinywaji vikali.

Mwingine alikuwa tipwatipwa, gauni limembana, nyonyo zimepigwa jeki zikichungulia. Kichwani alikuwa na wigi. Macho yake yalikuwa malegevu, si kwa kuumbwa lakini kilevi kilijenga taswira nyingine machoni kwake. Mwanaume yeyote ambaye angekutana na ulaghai ya macho yake yaliyo katika uso ulio wa kuvutia, basi asingesita kutaka kummiliki japo kwa muda ili amfaidi atakavyo.

Vinywaji walivyoagiza wanawake wale vilikuwa vya bei mbaya. Walionesha wazi kushindana kumchuna na wakati huohuo walionekana kumshobokea. Hakuwa na haja nao zaidi ya kampani yao tu.

Wakiwa wanaendelea kunywa, simulizi za tukio la ujambazi usiku uliotangulia iliibuka. Watu kadhaa, wakiwamo hao wanawake aliokuwa nao mezani, walisimulia kwamba katika tukio hilo, jambazi mmoja aliuawa na askari mmoja kujeruhiwa. Msako dhidi ya majambazi hao unaendelea sambamba na msako wa wageni waishio nchini kinyume cha sheria. Alisikiliza bila kuchangia hoja wala kuuliza swali, upande mmoja akitamani wakomeshe simulizi hiyo. Upande mwingine akitamani kudaka taarifa zaidi ya asichokijua, hasa kilichojiri baada ya tukio lile. Alikuwa na uhakika sasa kuwa moja kati ya risasi alizofyatua ilikuwa imeondoka na roho ya mtu.

Saa tatu baadaye alihama hoteli hiyo na kwenda sehemu nyingine na mmoja wa wanawake hao, yule tipwatipwa aliyekuwa amejitambulisha kwa jina la Mai, akimganda kama ruba, akijilengesha na kumshawishi kufanya ngono. Kichwa cha Pierre hakikuwa na wazo hilo kabisa. Mwili haukuitikia kwa namna yoyote ile.

Walikwenda kwenye maduka ya nguo ambako alinunua mashati matatu, suruali tatu, jaketi moja. Mwanamke yule aliambulia suruali ya jinzi na blauzi. Waliagana na kuahidiana kukutana jioni, ndani ya hoteli waliyokutana asubuhi. Kisha alijipumzisha kwenye bustani ufukweni mwa Ziwa Victoria, na hapo aliweza kuyaona vizuri mawe ya Bismark yaliyopangana na kuwa kivutio kikubwa. Kulikuwa na watu kadha wa kadha waliokuwa wakipunga upepo, wengine wakipiga picha.

Ilipotimu saa kumi na mbili za jioni Pierre alirejea kwenye nyumba aliyofikia kule milimani. Alikuta mlango umefungwa kama alivyouacha asubuhi. Alilifungua kufuli na kuingia ndani taratibu kama vile sakafu inatitia. Aliliendea begi lake. Lilivyokuwa sivyo alivyokuwa ameliacha asubuhi. Lilikuwa limesogezwa na zipu ilikuwa imefunguliwa kidogo, "Mh, begi langu limepekuliwa!" alinong'ona, kijasho kikijiunda katika paji la uso.Alichutama kulitazama vizuri, akifungua zipu kwa mkono wa kulia na kulitanua. Aliitwaa bastola na kuitachunguza kwa makini kisha kuirudisha, akafunga zipu na kutoka nje. Alimkuta Makubi, ameketi kwenye jabali.

Makubi aliinua macho, tabasamu hafifu likijiunda usoni, "Karibu jamaa yangu?" sauti yake ilikuwa nzito ya kukoroma kama ilivyokuwa usiku uliotangulia.

"Ahsante…" Pierre aliketi kwenye jabali lile kando yake, akimkazia macho mithili ya mtu aliyekuwa akitafuta majibu kwa maswali.

"Mbona umehamanika?" aliuliza kwa sauti tulivu, sauti yenye lengo la kutafuta muafaka.

"Begi langu limepekuliwa japo nilifunga mlango kwa kufuli."

Ulipita ukimya wa sekunde kadhaa Makubi akainua kope zake kumtazama Pierre, "Ni mimi niliyepekua!" alisema akizishusha kope zake ikiwa ni dalili ya kukionea haya kitendo kile. Zikapita sekunde kadhaa za ukimya kisha akasema, "Eh bwana eeh! Kumbe unamiliki chuma?"

Pierre alimkazia macho. Aliitikia kwa sauti ya chini, "Ndiyo."

"Cha nini mshikaji wangu?"

"Unauliza maswali mengi?" aliinuka toka kwenye jabali akasimama mkabala naye.

"Hakuna tatizo msela wangu, shwari tu." Alibaini kuwa mgeni huyu hakutaka kuendelea kuongelea silaha aliyoimiliki, akabadili mada. "Kwa hiyo unaondoka kesho kama ulivyosema?"

"Ndiyo, naondoka kesho…" alisita kama vile aliyekuwa akitafuta namna ya kuyapangilia vizuri maneno yake akimkazia tena macho Makubi. Kwa mwonekano Makubi hakuwa boya. Alionekana kuwa mtu mtata, mwerevu na pengine mwenye kujua vichochoro vyote. "Je, nitapata sehemu ya kuiacha. Namaanisha pa kuitunza."

"Nini?"

"Bastola. Sitaki kusafiri nayo."

"Mmmh..."Makubi alikuna kichwa, macho yakitazama mbali, "Utapata mshikaji wangu."

Baadaye alielekezwa kwa mtu ambaye aliishi maeneo ya hukohuko milimani, kwa Bob—mwenye umri wa miaka arobaini, mtanashati, asiyefanana na huduma hiyo aliyokubali kuitoa. Mtu huyu alikuwa tayari hata kuinunua endapo angekuwa anaiuza. Hakuwa na mpango wa kuiuza hivyo aliiacha hapo kwa makubaliano kwamba atarudi kuichukua. Alitakiwa kulipa kitunzio ambacho alikilipa bila ubishi.

~~~
~~~

Alfajiri ya siku iliyofuata, Pierre Businge alikuwa miongoni mwa abiria katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Nyegezi, akiwa safarini kuelekea Dar es Salaam. Huko alijua angeweza kuishi maisha ya utulivu. Alishakata shauri kurejea kwenye fani ya muziki, ambako pamoja na kipaji chake kikubwa cha kuimba, akipanga kwenda kupiga *drums* kwani kuimba kungemwanika wazi.

# 5

Ilikuwa ni burudani ya kukata na shoka, muziki ukitumbuiza,mamia ya watu wakisakata rumba kwa furaha. Kisha baada ya saa nzima ya bandika-bandua ukawadia wakati uliokuwa ukisubiriwa na kila shabiki aliyekunwa na burudani; wakati wa kuwatambulisha nyota wapya waliojiunga na bendi hii maarufu ya Sisi Musica.

Majuma mawili yalikuwa yamekatika tangu Pierre ahamie jijini Dar es Salaam na kujiunga na bendi hii. Haikuwa ngumu kwake kukutana na raia wa Kongo waishio Dar es Salaam. Alijitambulisha kwao na walipomsahili na kusikia kuwa alikuwa akitokea Bukavu na kuonesha kuwa aliwahi kuishi jijini Kinshasa, akipiga *drums* katika bendi, walimkaribisha katika bendi ya Sisi Musica. Hii ilikuwa mojawapo ya bendi zenye wanamuziki wa asili ya Kongo. Makazi yake ya muda yakawa Mwanayamala kwa Kopa, akiishi fleti moja na Allen Mutwashi almaarufu 'Daladala the Boss', mwimbaji nguli wa bendi hiyo.

Pierre alikuwa miongoni mwa wanamuziki watatu waliokuwa watambulishwe. Ingawa hakulipenda zoezi hilo, wamiliki wa bendi walisisitiza jambo hili kwa kuwa hiyo ndiyo ilikuwa desturi yao—kuwatambulisha wanamuziki wapya mara wanapojiunga.

Utambulisho huo ulifana sana, Pierre alitambulishwa kwa jina la Rish Kabasele. Alionesha umahiri wake wa kucharaza *drums*. Ulipigwa muziki mzito, mashabiki wakapagawa. Wanahabari waliohudhuria burudani hiyo waliandika habari za burudani walichukua picha za matukio mbalimbali. Hawakusita pia kufanya mahojiano na wadau waliohudhuria hapo; wote walimmwagia sifa Rish Kabasele. Shuhuda zilitoka, na kuna mmoja aliwahi kumwona enzi akiwa na Viqee la Musica.

"Namfahamu Rish tangu Kinshasa, wakati ule akiwa kijana mdogo. Hata Koffi Olomide alitaka kumwajiri katika bendi yake. Uwezo wake ni mkubwa, anaweza kupiga katika bendi yoyote, kama vile, Wenge Musica BCBG, na Fally Ipupa," alisema shuhuda.

Maisha mapya yalikuwa yameanza kwa Pierre Businge. Dar es Salaam ilikuwa raha, amani, utulivu. Siku za kutumbuiza zilikuwa tatu kwa juma—Ijumaa, Jumamosi na Jumapili. Walikuwa wakitumbuiza katika kumbi za Mango Garden, Msasani Club na Dar Live. Mazoezi yalifanyika mara tatu kwa juma katika siku ambazo walikuwa wamekubaliana.

Pierre hakuwa na papara ya kutumia akiba yake iliyotokana na dili za magendo ya silaha na madini iliyohifadhiwa katika akaunti yake ya Federal Bank.

Alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kuchangamkia huduma ya *Internet Banking*, na alipomiliki simujanja kutokana na kazi ya muziki, alifanya miamala iliyomwezesha kupanga fleti, Sinza, na kununua samani za ndani.

Kwa mara ya pili tangu ahukumiwe hukumu ile ya kifo nchini Kongo, aliingia katika baruapepe yake. Akakutana na moja iliyoandikiwa na Mo. Aliifungua na kuisoma. Palikuwa na ujumbe: *Uko wapi nikutafute?* Mo alikuwa na namna yake ya kuwasilisha jambo. Kadiri alivyoandika au kusema machache, kulimaanisha mengi zaidi. Akaijibu baruapepe hiyo ambayo ilibadilisha maisha yake.